


Fair Housing ni nini?



Sheria ya Makazi ya Haki ni sheria ya Serikali kuu ambayo inalinda haki yako ya:

- **Kuchagua nyumba** kwa bei unayo-imudu, hakuna ubaguzi
- **Kuchagua nyumba au kitongoji cha kuishi** bila vikwazo au kuendeshwa
- **Kuwa na fursa sawa** ya makazi, mikopo ya nyumba, tathmini, au bima
- **Kupokea vigezo**, masharti na huduma sawa kuhusu makazi yako
- **Upatikanaji sawa**—ikiwa wewe ni mtu mwenye ulemavu, una haki ya kuomba **malazi yanayofaa (utofauti)** katika sheria, sera, desturi, au huduma na/au **marekebisho yanayofaa** ili kuifanya nyumba yako iweze kufikika
- **Uhuru** dhidi ya usumbufu au kutishwa kwa kutumia haki zako za makazi ya haki.

Majiji na miji lazima pia ifuate sheria za Fair Housing wakati wa ujenzi, kuweka, kuendeleza na kupanga makazi katika vitongoji. Serikali za Mitaa huamua aina za makazi na ukanda unaoruhusiwa na lazima zifanye kazi kikamilifu ili kuondoa ukabila na ubaguzi wa nyumba.



Iapo unafikiri umebaguliwa katika miamala ya nyumba, wasiliana na:

Umoja wa Makazi wa Northwest (Northwest Fair Housing Alliance)
25 W Main Ave., Suite 250
Spokane, WA 99201
509-325-2665
1-800-200-FAIR (3247)
Faksi: 1-866-6308

NWFHA inaweza kukushauri kuhusu machaguo yako na kukutetea. Huduma zetu ni bure. Ofisi yetu inawajibika.



Kazi ambayo ilitoa msingi wa chapisho hili iliungwa mkono kwa kiasi na ufadili wa Idara ya Makazi na Maendeleo ya Miji ya Marekani (U.S. Department of Housing and Urban Development), HUD. NWFHA inawajibika hasa na usahihi wa taarifa na tafsiri zilizomo katika chapisho hili. Swahili— 6/2022



(509) 325-2665
1-800-200-FAIR (3247)
www.nwfairhouse.org

Sheria ya Fair Housing zinakulinda dhidi ya ubaguzi katika miamala ya makazi kwa sababu ya:

Jamii yako
Rangi yako
Asili yako ya Kitaifa
Dini yako
Jinsi / Jinsia
Ulemavu wako
Hadhi ya Familia yako

Haya yanaitwa "Matabaka Yanayolindwa."



Hatua zifuatazo zikichukuliwa kwa sababu ya "tabaka lako linalolindwa" ni kinyume cha sheria

- Kukataa kukuuzia au kukupangisha
- Kubaguliwa katika vigezo, masharti, au upendeleo wa uuzaaji au ukodishaji
- Kukwambia kwamba nyumba haiuzwi wala kupangishwa ilhali inauzwa au inapangishwa
- Kukushawishi kuuza au kupangisha nyumba yako kwa sababu watu wa jamii, rangi, asili ya taifa fulani, n.k. wanahamia jirani.
- Kutoa matangazo au kauli za kibaguzi dhidi ya tabaka lako linalolindwa.

Fair Housing inakulinda wakati:

Kununua



Kukopa



Kupanga



Bima



Kuweka ukanda

